# MWONGOZO WA
# KANUNI ZA MASHINDANO
## TANZANIA BASKETBALL FEDERATION
## 2024

IMEANDALIWA NA:
KAMISHENI YA UFUNDI NA MASHINDANO (TBF)
EMAIL: INFO@TBF.OR.TZ


NI ZAIDI YA GAM
CRDB BANK

# TABLE OF CONTENTS


1. UTANGULIZI ..... 3
2. MADHUMUNI YA KUANDAA KANUNI ZA LIGI ..... 3
3. MATUMIZI NA TAFASIRI ..... 3
4. TIMU SHIRIKI ..... 4
5. USIMAMIZI WA SHINDANO ..... 4
6. MTINDO WA KUCHEZA ..... 4
7. KUSHUKA DARAJA ..... 4
8. MSHINDI WA LIGI (MSIMAMO WA LIGI) ..... 6
9. RATIBA YA LIGI ..... 6
10. TARATIBU ZA MCHEZO ..... 6
11. USAJILI WA WACHEZAJI, WALIMU NA VIONGOZI WA TIMU/KLABU ..... 7
12. WACHEZAJI WASIOKUA RAIA WA TANZANIA ..... 8
13. ADA NA VIINGILIO ..... 8
14. UHAMISHO WA MCHEZAJI ..... 9
15. WACHEZAJI HURU ..... 9
16. ZUIO LA USAJILI ..... 10
17. WAKATI WA MCHEZO NA PINDI MCHEZO UKIENDELEA ..... 10
18. ADHABU ..... 10
19. SARE ..... 12
20. WAAMUZI ..... 12
21. UDHIBITI WA VILABU, TIMU NA WASHABIKI ..... 13
22. RUFAA NA MALALAMIKO ..... 14
23. USIKILIZAJI WA RUFAA/MALALAMIKO NA TAMKO LA KAMATI/BODI ..... 15
24. UDHALILISHAJI WA NEMBO(BRAND), JINA LA CHAMA AU VYAMA VISHIRIKI NA MDHAMINI. ..... 16
25. USIMAMIZI/UTEKELEZAJI WA ADHABU ..... 16
26. USIMAMIZI WA MCHEZO. ..... 16
27. HUDUMA YA KWANZA NA AFYA ..... 17
28. KUFUTA KANUNI NA MAMBO YASIYOKUWEPO KWENYE KANUNI ..... 17
29. DOKEZO ..... 17

## 1. UTANGULIZI
Shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania (TBF) ndio chombo chenye mamlaka ya usimamizi wa mchezo wa mpira wa kikapu Tanzania.

Shirikisho limeandaa kupitia kamisheni zake mwongozo wa kanuni za kuendeshea mashindano mbali mbali ya mchezo wa mpira wa kikapu ambao utatoa mwongozo mmoja wa kitaifa kwenye maeneo yote yahusuyo mchezo kuanzia kwenye usajili, sheria za mchezo, usimamizi, ushiriki, adhabu na mambo menginyo ya kuzingatia katika mchezo.

Mwongozo huu utatumiwa na vyama vya mikoa na wadau wote nchini.

## 2. MADHUMUNI YA KUANDAA KANUNI ZA LIGI
Lengo la huu mwongozo ni kutoa mazingira sawa ya ushindani na usimamizi wa mchezo ili :-

2.1. Kuondokana na migogoro isiyokuwa ya lazima katika uendeshaji wa ligi Tanzania nzima.
2.2. Kuwa na Ligi zilizo bora zaidi, ambazo zitaweza kuleta ushindani kwa timu shiriki na pia kutoa burudani zaidi kwa watazamaji, pamoja na kuchochea wadhamini zaidi kujitokeza kwa ajili ya kudhamini ligi na timu shiriki.
2.3. Kuwezesha kupata wachezaji, waamuzi, walimu bora kinidhamu ili kuwezesha mchezo wa mpira wa kikapu kuwa na ubora wa juu kabisa nchini.

## 3. MATUMIZI NA TAFASIRI
Kanuni hizi isipokuwa pale ambapo imeainishwa vinginevyo zitatumika kwa timu za wanawake na wanaume.

### 3.1. TAFASIRI:
- **FIBA:** Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Kikapu
- **BMT:** Baraza la Michezo Tanzania
- **TBF:** Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania
- **TBCA:** Chama cha Walimu wa Mpira wa Kikapu Tanzania
- **TBRA:** Chama cha Waamuzi wa Mpira wa Kikapu Tanzania
- **OBR:** Sheria za Mpira wa Kikapu
- **OBRI:** Ufafanuzi wa Sheria za Mpira wa Kikapu
- **KAMATI TENDAJI:** Kamati ya Utendaji ya TBF
- **LIGI:** Ligi ya mpira wa Kikapu.
- **KLABU:** Klabu ya mpira wa Kikapu
- **TIMU:** Timu ya mpira wa Kikapu.
- **MPIRA:** Mpira wa Kikapu
- **MCHEZO:** Mchezo wa Mpira wa Kikapu
- **CHAMA:** Chama cha mpira wa Kikapu.
- **SERIKALI:** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- **MSHABIKI/WASHABIKI:** mtu yeyote anayefuatilia maendeleo ya mchezo (uwanjani au nje ya uwanja)

## 4. TIMU SHIRIKI

Timu shiriki lazima ziwe zimekidhi vigezo vyote vya uhai wa timu au Klabu ili kushiriki ligi kama ifuatavyo: -

4.1. Timu/Klabu lazima iwe imesajiliwa na BMT
4.2. Timu/Klabu lazima iwe imemaliza madeni na kulipia ada zake zote husika kwa taasisi husika za mchezo. Mfano Vyama vya Mikoa, BMT, N.K.

## 5. USIMAMIZI WA SHINDANO

5.1. TBF kupitia vyama vya mikoa na kurugenzi husika ndiyo wakatao simamia mashindano yote ya Basketball Tanzania nzima.
5.2. Kupitia TBF vyama vishiriki vitakua na majukumu ya kusimamia walimu na waamuzi ili kusimama katika misingi bora ya mpira wa Kikapu.
5.3. TBF na vyama vyote vishiriki vitakua na jukumu la kuhakikisha Timu/Klabu zote zinafuata sheria za FIBA na kanuni zilizowekwa na TBF.

## 6. MTINDO WA KUCHEZA

6.1. Timu zote zitacheza mizunguko miwili (2) kwa mtindo wa nyumbani na ugenini (Home and Away) kulingana na urefu wa ligi na wingi wa timu.
6.2. Baada ya kumaliza mzunguko timu nane (8) za juu (Kwa ligi yenye timu zaidi ya nane) zitaingia hatua ya robo fainali na kwa ligi yenye timu chache timu nne (4) za juu zitacheza Nusu Fainali kwa idadi ya mechi 3,5 au 7 kulingana na pendekezo la kamati husika ya ligi.
6.3. Namna ya kucheza robo fainali na nusu fainali ni

6.3.1. **Robo fainali**

Mshindi 1 vs Mshindi 8
Mshindi 2 vs Mshindi 7
Mshindi 3 vs Mshindi 6
Mshindi 4 vs Mshindi 5

6.3.2. **Nusu Fainali**

Mshindi 1 vs Mshindi 4
Mshindi 2 vs Mshindi 3

6.3.3. Mshindi wa Tatu utachezwa mchezo mmoja (1) tu.
6.3.4. Fainali itachezwa michezo 3,5 au 7 kulingana na makubaliano ya kamati husika ya ligi ya mkoa.

## 7. KUSHUKA DARAJA

Kwa mikoa ambayo ina fuata mtindo huu basi timu mbili za mwisho zitashuka daraja na timu mbili zilizoongoza ligi daraja la kwanza au ligi za kanda zitapanda daraja na kucheza ligi kuu.

**NB:** Hakuna timu za ligi ya wanaake zitakazoshuka daraja.

# Maandalizi ya Mashindano



## 8. MSHINDI WA LIGI (MSIMAMO WA LIGI)

Ili kupata namba 1-8 au 1-4 katika msimamo wa ligi zitatumika sheria za FIBA ambazo ni za wakati husika.

## 9. RATIBA YA LIGI

9.1. Tarehe ya kuanza kwa ligi na kumalizaika kwa ligi zote itatolewa na kamati ya utendaji ya TBF.

9.2. Vyama vya mikoa na kurugenzi husika vitatakiwa kuhakikisha kwa muda uliotolewa na TBF ligi inaanza na kuisha ndani ya muda huo.

9.3. Utengenezaji wa ratiba ya ligi utatolewa na kurugenzi ya ufundi na mashindano ikishirikiana na kamati la ligi katika mkoa husika.

9.4. Ratiba itatolewa wiki mbili au zaidi kabla ya Ligi kuanza.

9.5. Ratiba ya ligi ikishatolewa haitobadilisha isipokua kama kuna dharura au sababu za msingi.

## 10. TARATIBU ZA MCHEZO

10.1. Kila mchezo lazima uwe na waamuzi wenye sifa **husika**, walimu wenye sifa **husika**, Kamisaa wa mchezo na Mkaguzi na Mdhibiti Ubora wa Waamuzi (Referee Assessor)

10.2. Kutakua na mkutano kati ya viongozi wa Timu/Klabu husika za michezo ya mwisho wa wiki. Mkutano huu utafanyika wiki moja kabla ya michezo hiyo kufanyika na itahusisha wafuatao: Viongozi wa timu husika, Makamisaa wa mchezo, Mkaguzi na mdhibiti ubora wa waamuzi (Referee Assessor)

10.3. Mtu yeyote atakayechelea kufika kwenye Mkutano tajwa hapo juu atawajibika kulipa faini itakayopangwa na kamati tendaji ya shindano husika.

10.4. Katika mkutano huo kama kuna timu ina udhuru basi ndo muda wa kufikisha udhuru wake yaani wiki moja kabla ya mechi husika kuchezwa. Sababu za kuahirisha zikiambatana na vielelezo lazma viwepo katika barua ya kuhairisha mchezo.

10.5. Mchezo ulio hairishwa utachezwa siku yoyote itakayokubaliana kamati na timu husika.

10.6. Mchezo unaweza kuhairishwa kwa lazima kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa binadamu kama kifo, mvua, kuwepo kwa zababu zozote zitakazo fanya wachezaji kushindwa kuona (giza, vumbi, ukungu).

10.7. Kutokana na sababu tajwa hapo juu, Mchezo utasubiriwa kwa dakika arobaini (40) kutengemaa kwa hali, muda ukiisha Mkurugenzi wa Ufundi ambaye ni Mwakilishi wa kamati ya chama husika na msimamizi mkuu wa mchezo atatoa uamuzi wa kuendelea au kutoendele kwa Mchezo husika.

10.8. Mchezo utaendelea pale ulikoishia kwa Kutumia Takwimu zilezile na Kumalizia muda uliosalia na matokeo ya awali hayatafutwa na Itakapobidi ndani ya masaa 48 na kiwanja tofauti na cha awali kinaweza kutumika kama zipo sababu za kufanya hivyo pamoja na kubadilisha waamuzi, Na wachezaji pia.

10.9. Kwa Kushauriana na Mwandaaji wa Shindano chama husika, Kupitia kurugenzi ya Ufundi na mashindano, mwamuzi ataagizwa kuahirisha mchezo wakati ukiendelea ikiwa hali ya usalama katika uwanja inaashiria uvunjifu wa amani ikiwemo mashabiki kuingia mara kwa mara uwanjani, kupigana, kurusha chupa na kumwaga maji uwanjani, au matumizi ya lugha chafu/matusi kwa washabiki.

10.10. Baada ya kuamua kuahirishwa kwa mchezo, ikigundulika ni washabiki ndio waliosababisha mchezo kuvunjika basi mchezo hautarudiwa na timu husika kwa vurugu hizo kunyimwa ushindi na ushindi utaenda kwa timu pinzani.

10.11. Wajumbe wa kamati husika ya ligi wasiopungua wawili watakaa siku hiyo hiyo na kwa kutumia taarifa ya Kamisaa wa mchezo na waamuzi, maamuzi yatatolewa haraka kwa kuzingatia taarifa hiyo.

10.12. Timu/wachezaji hazitakiwi kupeana mikono kabla ya mchezo na baada ya mchezo. Hii ni kwa sababu ya kuzingatia namna mojawapo ya kujinginga na maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO 19.

## 11. USAJILI WA WACHEZAJI, WALIMU NA VIONGOZI WA TIMU/KLABU

11.1. Kila Mchezaji, Mwalimu (kocha), Daktari, Mwamuzi na Meneja wa timu Ili waweze kushiriki katika shindano wanalazimika kupata leseni ya usajili kwa mujibu wa taratibu, sheria na Kanuni zitakazokuwa zimeandaliwa na Chama cha Mkoa kwa mwaka husika ambapo watatakiwa kusajiliwa katika mfumo wa TBF Map unaotambuliwa na FIBA utakaombatana na ada ya shilingi 5,000 kwa kila mmoja.

11.2. Usajili wa wataalamu kama daktari, waamuzi na makocha watahitajika kuwakilisha vyeti vyao.

11.3. Gharama ya ada ya leseni ya mchezaji, Mwalimu na Mwamuzi itakuwa ni ya kila msimu.

11.4. Wachezaji wote watalazimika kuwasilisha taarifa zifuatazo wakati wa usajili kwa njia ya mfumo wa TBF Map (i.e., Picha, Cheti cha kuzaliwa kama ana umri chini ya miaka 18, Hati ya kusafiria kama ni mchezaji wa kigeni, Kitambulisho cha NIDA, Fomu ya Dakitari na Mkataba wa mchezaji)

11.5. Watakaohusika kwenye usajili ambao pia ndiyo watakaoruhusiwa kukaa kwenye bench kwa msimu wote ni kama wafuatao-

a. Kocha mkuu
b. Kocha Msaidizi no 1
c. Kocha Msaidizi no 2
d. Meneja wa Timu
e. Daktari wa timu (Awe na vielelezo vinavyomtabulisha kuwa ni daktari) au mtoa huduma ya kwanza.
f. Watunza takwimu wawili (Wawe wamesomea ujuzi huo au wanauelewa na kazi hiyo)

11.6. Kila timu/Klabu itatakiwa kusajili wachezaji wasiopungua saba (7), na wasiozidi ishirini (20) hadi ifikapo siku ya mwisho wa tangazo au barua ya Chama ilivyoelekeza.

11.7. Wachezaji, Walimu, na wahusika wote watakaosajiliwa na Timu/Klabu ni lazima wakamilishe usajili kupitia mfumo wa usajili wa TBF unaotambulika na FIBA http://map.tbf.or.tz/ utakaosimamiwa na chama husika cha mkoa.

11.8. Kila timu/klabu inapaswa kuwapima wachezaji wake waliosajiliwa na kuthibitisha kuwa wana afya njema ya kushiriki katika ligi au mashindano ya chama. Uthibitisho huo uambatanishwe wakati wa usajili wa wachezaji unapofanyika.

## 12. WACHEZAJI WASIOKUA RAIA WA TANZANIA

12.1. Wachezaji ambao si Raia wa Tanzania, Pia ambao wanatoka nje ya nchi wataruhusiwa kucheza wakiwa na kibali maalumu cha serikali kinacho mruhusu kucheza nchini Tanzania, hati ya kusafiria na Lesseni kutoka FIBA ya kumruhusu kucheza.

12.2. Timu/Klabu Inaruhusiwa Kusajili wachezaji wasiokuwa Raia wa Tanzania wasiozidi watano (5).

12.3. Timu/Klabu itaruhusiwa kutumia wachezaji **wote watano (5**) kwa mchezo mmoja watakaoorodheshwa katika karatasi za matokeo (Score sheet) na wanatakiwa kuwemo uwanjani kwa pamoja ni wachezaji watatu (3) tu.

12.4. Ada ya Usajili kwa Wachezaji wasiokuwa Raia wa Tanzania **haitokuwa sawa na ile ya mchezaji ambaye ni raia wa Tanzania.Ada hii itapangwa na chama husika kutokana na mazingira husika. Leseni yake italipiwa kiasi cha shilingi 50,000 kwenye mfumo wa FIBA/TBF MAP.**

12.5. Wachezaji wa Tanzania wanaocheza ligi nje ya Tanzania wataruhusiwa kucheza ligi ya Tanzania ili kuleta motisha kwa watanzania wenzao ila nao watasajiliwa kama wachezaji kutoka nje ya Tanzania (Wachezaji wa Kigeni).

## 13. ADA NA VIINGILIO

Kutakuwa na Ada na Viingilio kama ifuatavyo

13.1. Ada ya mwaka ya Klabu/timu kwa chama cha mkoa husika.

13.2. Ada ya Timu kwa ajili ya kujisajili/Kiingilio katika ligi (i.e.kwa mkoa husika kama ni ligi ya mkoa).

13.3. Ada ya wachezaji wa ndani, wachezaji wa kigeni, waamuzi, walimu wa timu na viongozi wa timu.

13.4. Ada ya Malalamiko

13.5. Ada ya Rufaa

Ada zote zilipwe kabla ya kuanza kwa msimu wa ligi. Ada na viingilio zitatozwa kulingana na makubaliano ya chama husika na wadau wake katika ligi.

Hakuna timu/klabu itakayopangwa katika ratiba na Mkurugenzi wa ufundi na Mashindano bila kukamilisha malipo au ada zake zote na usajili wa wachezaji pamoja na viongozi.

## 14. UHAMISHO WA MCHEZAJI

14.1. TBF itaratibu uhamisho wa wachezaji kwa kushirikiana na vyama vya mikoa kwa utaratibu na mgawanyo ufuatao: -

14.1.1. **Uhamisho ndani ya mkoa:** Utasimamiwa na mkoa husika isipokuwa ada ya leseni italipiwa kubadilisha taarifa za mchezaji.

14.1.2. **Uhamisho wakati wa ligi ya taifa:** Utasimamiwa na TBF na utagharimu 30,000/- na mgawanyo wake utakuwa na uwiano wa 10,000/- TBF na Mkoa aliochezea ligi utapata 20,000/-.

14.1.3. **Uhamisho wakati wa taifa cup:** Utasimamiwa na TBF na mgawanyo wake utakuwa 30,000/- na mgawanyo wake utakuwa na uwiano wa 10,000/- TBF na Mkoa aliochezea ligi utapata 20,000/-.

Gharama iliyo ainishwa inahusu ada ya uhamisho ("clearance fee") ambayo ni nje ya gharama ambazo mchezaji ameingia binafsi kati ya Klabu na Klabu au Mkoa na Mkoa.

14.2. TBF itaruhusu uhamisho pale timu mchezaji anapohitajika kuhamishwa/kuhamia timu inayo kwenda cheza mashindano ya kimataifa. Kutoka timu moja hadi nyingine ndani ya mkoa kutasimamiwa na mkoa na ruhusa ya TBF.

14.3. Uhamisho wa wachezaji utafanyika kulingana na dirisha la usajili. Hakutakuwa na uhamisho wowote wa mchezaji katikati ya msimu unao endelea.

14.4. Vielelezo husika wakati mchezaji anapohama timu.

14.4.1. Barua ya timu inayomuhitaji mchezaji.

14.4.2. Barua toka timu aliyochezea yenye kibari cha kumruhusu kwenda kucheza timu inayomuhitaji.

14.4.3. Barua zote ziwe zimesainiwa na katibu na muhuri wa timu.

14.4.4. Barua hizo ziambatane na ada husika kwa mkurugenzi wa ufundi zikiwa zina nakala Tatu (Klabu/Team, Chama cha mkoa, TBF.)

14.4.5. Mchezaji yeyote ambaye hatafuata utaratibu huu hataruhusiwa kucheza na kuondolewa kwenye usajili wa timu husika.

## 15. WACHEZAJI HURU

15.1. Mchezaji yeyote ambaye hakusajiliwa na Klabu/Timu yoyote ya Daraja lolote katika msimu uliopita atakua huru, hahitaji uhamisho bali atalipiwa ada ya usajili.

15.2. Mchezaji yeyote ambaye Klabu/Timu yake imesitisha mkataba wake/au mkataba wake umemalizika, atakua mchezaji huru na hivyo hatalipiwa ada ya uhamisho isipokuwa ada ya usajili.

15.3. Mchezaji aliyerudi nyumbani baada ya kumaliza mkataba wake nje hatokuwa huru, hadi atakapokamilisha taratibu za uhamisho wa Kimataifa.

## 16. ZUIO LA USAJILI

Chama kina uwezo wa kuzuia Usajili wa Timu/Klabu yoyote ambayo kitaona haukukamilika mfano kutuma/Kuwasilisha taarifa za usajili ambazo hazikosahihi kwa mujibu wa miongozi na kanuni za ligi au hazijajazwa kwa ukamilifu au kucheleweshwa bila sababu za msingi.

## 17. WAKATI WA MCHEZO NA PINDI MCHEZO UKIENDELEA

Viongozi husika na mchezo wa siku hiyo wata fuata sheria na taratibu zote zilizopo kwenye FIBA RULE BOOK (Official Basketball Rules) Ambayo ni ya sasa(current) ili kuweza kuusimamia mchezo na kuamua jambo lolote linalohusiania na mchezo kama yafuatayo:

17.1. Muda wa timu kufika uwanjani/Timu kutokufika uwanjani.

17.2. Kuchelewa kuwasilisha majina kwa waamuzi wa mezani.

17.3. Kutotimi aidadi ya wachezaji watano.

17.4. Jezi kutotimia, kutofautiana au kufanana.

17.5. Nidhamu katika benchi (ikiwemo idadi ya watu wanaotakiwa kukaa kwenye benchi).

## 18. ADHABU

18.1. Mchezaji yeyote atakaetolewa nje moja kwa moja (**Disqualified foul**) ataadhibiwa kulingana na kanuni za ligi ya mkoa husika zilivyo ainishwa.

18.2. Mchezaji akipata (**disqualified foul)** iliyotokana na **Technica foul na Unsportsman foul** au **Technical foul mbili**/ **Unsportsman foul mbili** ataadhibiwa kulingana na kanuni za ligi ya mkoa husika zilivyo ainishwa na pamoja na kulipa fine itakayo ainishwa kwenye kanuni za mkoa husika.

18.3. Mchezaji atakayepata Technical 3 au Unsportsman 3 katika michezo mitatu tofauti-atafungiwa kucheza mchezo mmoja unaofuata pamoja na kulipa fine itakayo ainishwa kwenye kanuni za mkoa husika.

18.4. Timu/klabu ambayo haitafika uwanjani kucheza mchezo wake kwa mujibu wa ratiba na bila kutoa taarifa au sababu za msingi kwa Mkurugenzi wa ufundi

18.4.1. Kwa mchezo wa kwanza na wa pili timu pinzani itapewa ushindi wa Alama 2 na magoli 20-00.Aidha timu/klabu hiyo itaadhibiwa kulipa kiasi cha fedha kilicho ainishwa na chama husika kwa kila mchezo ambao timu haikufika uwanjani.Na faini hiyo ilipwe kabla ya mchezo unaofuata.

18.4.2. Kwa mchezo wa tatu mfulilizo, timu hiyo itaondolewa katika ligi/shindano na kuadhibiwa kulipa kiasi cha fedha kilicho ainishwa na chama husika pamoja na adhabu nyingine ya ziada chama kikiona itafaa kutolewa.

18.5. Timu/klabu itakayotumia/kumchezesha mchezaji ambaye hakusajiliwa / hakukamilisha usajili na kubainika, timu hiyo kama itashinda mchezo huo itanyanga'nywa ushindi na kupewa timu pinzani kwa kupewa Alama 2-0.

# Sare za Timu



18.7. Endapo itakugundulika na kuthibitika kuwa timu/klabu imemtumia mchezaji aliyesajiliwa mara mbili katika mkoa husika au katika timu/Klabu mbili tofauti za ligi za mikoa tofauti, basi Klabu/timu hizo zitafutiwa matokeo michezo yote aliyocheza mchezaji huyo na pia Mchezaji huyo atafutiwa usajili na hataruhusiwa kucheza msimu husika mahali popote nchini Tanzania.

## 19. SARE

Utaratibu wa Sare utafuata Sheria za FIBA ikiwemo na hizi zifuatazo:

19.1. Wachezaji wanatakiwa kuvaa jezi zilizotolewa na mdhamini au jezi za timu zao, au jezi kutoka kwa mdhamini wake zinazokubaliwa na sheria za FIBA.

19.2. Ni lazima wachezaji wote wavae soksi nyeupe/nyeusi/ zinazofanana na jezi walizovaa mda wote wa mchezo. Mchezaji hatoruhusiwa kucheza/kuingia uwanjani kama hatakuwa amevaa soksi zinazokubaliwa kwa mujibu wa kanuni.

19.3. Namba za jezi zifanane (Juu na chini)

19.4. Mchezaji haruhusiwi kuvaa fulana ndani ya sare hata kama inafanana isipokuwa kwa kibali maalum.

19.5. Skin tight lazima zifanane kwa rangi, endapo hazitafanana ni wajibu wa kwenda kubadili na kubaki na jezi sahihi.

19.6. Team officials wote, wanatakiwa wawe katika sare na wakiwa nadhifu, hawataruusiwa kuvaa kaptula au pensi wala kuvaa viatu vya wazi muda wote wanapokuwa kwenye benchi.

19.7. Vazi la Truck suit linaruhusiwa kuvaliwa wakati unaposimamia benchi mda wote wa mchezo.

## 20. WAAMUZI

20.1. Mkurugenzi wa Kamisheni ya waamuzi akishirikiana na chama cha waamuzi cha mkoa husika watateua majina ya waamuzi wa ndani, waamuzi wa mezani na kamisaa na kupeleka majina kwenye bodi kwa uthibitisho.

20.2. Uchaguzi wowote wa waamuzi watakaochaguliwa kuchezesha michezo yoyote katika ngazi yoyote (i.e., bonanza, ligi za mikoa, ligi ya taifa na mashindano ya Taifa Cup) utazingatia vigezo vifuatavyo: -

20.2.1. **Ujuzi** – ngazi ya cheti alichosomea (**Level 1** – Bonanza, Ligi za mikoa, **Level2** - Ligi za mikoa hatua za mtoano, Taifa Cup, Ligi ya Taifa, **National/FIBA** - Mashindano ya kimataifa, Hatua za mtoano Taifa Cup na NBL)

20.2.2. **Uzoefu** – idadi ya michezo aliyokwisha chezesha.

20.2.3. **Ripoti** ya usimamizi wa viwango na ubora (i.e., Referee assessment & performance reports)

20.3. Hakuna timu/Klabu itakayokuwa na uwezo wa kupinga au kukataa mwamuzi yeyote aliyepitishwa na bodi kuchezesha ligi ingawaje TBF inaweza kuingilia hili swala kwa kuzingatia taswira na hamasa ya mchezo.

20.4. Mkurugenzi wa Ufundi atakuwa na jukumu la kuteua Mkaguzi na mdhibiti viwango vya waamuzi (Referee Assessor) kwa makubaliano kati ya chama cha waamuzi mkoa, Mkurugenzi wa waamuzi na vilabu vinavyoshiriki.

20.5. Mkaguzi na mdhibiti viwango vya waamuzi (Referee Assessor) atakuwa na jukumu la kuangalia viwango na nidhamu ya waamuzi wakati wote wa mchezo na kutoa ripoti yake kwa Mkurugenzi/Kamisheni ya ufundi mkoa, Kamisheni ya waamuzi mkoa, Kamisheni ya waamuzi TBF na chama cha waamuzi TBRA.

20.6. Kwa mwamuzi, mwamuzi wa mezani na kamisaa atakayefanya ishara za matusi au lugha mbaya kwa wachezaji viongozi wa timu na mashabaki ata pelekwa kamati ya nidhamu ya chama cha waamuzi cha mkoa husika kisha ripoti kwenda kwa Kamisheni ya waamuzi mkoa, Kamisheni ya waamuzi TBF na chama cha waamuzi TBRA ambapo adhabu ya mwisho itatolewa na TBF kama wasimamizi wa mchezo kitaifa.

## 21. UDHIBITI WA VILABU, TIMU NA WASHABIKI

21.1. Ikigundulika na kuthibitika kwamba washabiki wa timu wakasababisha mpira kutoendelea/ kuvunjika /kusimama na kuathiri mda wa mchezo kwa kutupa chupa uwanjani, kumwaga maji uwanjani, kuingia uwanjani kwa lengo la kushambuliwa wachezaji/mwamuzi. Timu husika itatozwa faini iliyokubaliwa na chama cha mkoa husika na kunyang'anywa ushindi na kupewa timu pinzani.

21.2. Ikigundulika na kuthibitika kwamba mchezaji yeyote aliesajiiwa kucheza ligi ya Mkoa, Daraja la kwanza au nyingineyo akitoa matusi kwa mwamuzi/mchezaji mwenzake awapo jukwaani atafungiwa michezo mitatu na kutozwa faini itatozwa faini iliyokubaliwa na chama cha mkoa husika.

21.3. Ikigundulika mshabiki yeyote anatoa matusi hadharani, lugha za kufedhehesha kwa kumshambulia Mchezaji, Mwamuzi, Mwalimu, Kiongozi wa Timu au mshabiki mwenzake kwa kujibizana. Watatolewa mara moja eneo la uwanja na Watafungiwa kuingia uwanjani kwa wiki tatu hii itachukuwa sheria za nchi kwa vyombo vya ulinzi na usalama.

21.4. Mchezaji yeyote akionyesha utovu wa nidhamu awapo uwanjani kwa lengo la kutaka kumuumiza mchezaji mwenzake (Mpinzani) kwa makusudi kwa kumpiga kiwiko, Ngumi au teke Atafungiwa michezo mitano (5) mfululizo na kutozwa faini iliyokubaliwa na chama cha mkoa husika.

21.5. Mchezaji akimshambulia mwamuzi kwa matusi/kumshambulia mwilini. Atafungiwa miezi sita (6) kutojiusisha na mchezo wa mpira wa kikapu ndani na nje ya nchi na kutozwa faini ya Tshs 300,000/=

21.6. Mchezaji yeyote awapo uwanjani au kwenye bench akitoa ishara ya matusi kwa namna yeyote ile kwa mashabiki, atafungiwa michezo miwili na kutozwa faini iliyokubaliwa na chama cha mkoa husika.

21.7. Ikitokea wachezaji wakapigana uwanjani. Sheria za FIBA zitafuatwa na watafungiwa miezi miwili (2) na faini kila mmoja kama ilivyokubaliwa na chama cha mkoa husika.
21.8. Kocha/kocha msaidizi akiishambulia meza/mwamuzi kwa matusi na kusababisha fujo atafungiwa miezi mitatu na kulipa faini kama ilivyokubaliwa na chama cha mkoa husika.
21.9. Kocha/kocha msaidizi /wachezaji /viongozi wa timu wakifanya fujo kwenye meza ya waamuzi na kusababisha uharibifu wowote wa vifaa vya mezani, watatoa gharama za utengenezaji na waatafungiwa miezi sita (6) na kutozwa faini tshs 300,000/=
21.10. Faini zote zitalipwa ndani ya kipindi cha adhabu uliyopewa hata kama utakuwa umemaliza adhabu hutaendelea kucheza au kukaa kwenye bench kama hujalipa faini uliyoandikiwa.
21.11. Endapo timu/Klabu itavunja kanuni au sheria na kusababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kuadhibiwa Mwamuzi au kiongozi, Mwamuzi husika na kamisaa watakabidhi taarifa ya maandishi kwa kamati ya ufundi na vivuli vyake kwenda kwa vyama husika ikiwemo TBF ndani saa ishrini na nne (24) baada ya mchezo kumalizika.
21.12. Ili kuwa na uhakika wa kutoa adhabu kwa kujiridhisha, na kubaini matukio ndani ya uwanja, kamera na video zitakazokua zimechukua tukio /matukio hayo zitatumika kama vielelezo.
21.13. Kiongozi au mtu yeyote hana mamlaka ya kutengua au kupinga adhabu inayotolea baada ya kukiuka kanuni zilizopo.
21.14. Kocha ni lazima aende kwa vyombo vya habari kwa ajili ya mahojiano. Ikifahamika kocha kukataa atatozwa faini kama ilivyokubaliwa na chama cha mkoa husika.
21.15. Hairuhusiwi kwa kiongozi wa timu, kocha na msaidizi wake, wachezaji pamoja na waamuzi kwenda kwa Mdhamini yeyote ataekuwa amedhamini shindano kwa lengo la kwenda kufanya maongezi yeyote yanayohusiana na udhamini wake. Ikigundulika na kufahamika kiongozi/mchezaji/mwamuzi huyo kufanya hivyo atafungiwa kwa muda wa msimu mzima (mwaka mmoja) kujihusisha na maswala ya mpira wa kikapu.

## 22. RUFAA NA MALALAMIKO

22.1. Pingamizi na rufaa ni lazima zitumwe na ziambatanishwe na malipo kwa Mkurugenzi wa Ufundi na Mashindano katika Mkoa husika.
22.2. Kamati ya ufundi na mashindano itatoa maamuzi ya rufaa na adhabu kama ilivyo kulingana na sheria za mchezo kwa mujibu wa FIBA na kanuni zilizopitishwa na chama cha mkoa husika.
22.3. Timu/Klabu itakayoona maslahi yake yanahujumiwa, inayo haki ya kuwasilisha malalamiko yake kuhusu hujuma hiyo. Malalamiko ya timu/klabu husika ni lazima yafuate taratibu na sheria za mchezo.

22.4. Malalamiko na vielelezo vyote vikiwa kwa maandishi vitumwe au viwasilishwe kwenye kamati ya rufaa si zaidi ya saa 24 baada ya mchezo husika kumalizika.
22.5. Ada pamoja na nakala tatu za malalamiko ziambatanishwe na kulipwa na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa ufundi.
22.6. Hakuna malalamiko yatakayo pokelewa/kusikilizwa baada ya saa 24 kupita, na kama (kifungu 22.4) hakijakamilika, matokeo yatabaki yalivyokuwa.
22.7. Hakuna fedha itakayo rudishwa hata kama mlalamikaji atashinda/Kushindwa malalamiko yake dhidi ya mpinzani wake.
22.8. Endapo timu/Klabu inapinga au inalalamikia maamuzi ya kamati ya ufundi, adhabu itabaki ilivyo hadi hapo jopo la rufaa litakapotoa maamuzi baada ya uchunguzi wake ndipo ibadilishwe au iendelee.

## 23. USIKILIZAJI WA RUFAA/MALALAMIKO NA TAMKO LA KAMATI/BODI

23.1. Upingaji au pingamizi kuhusiana na malalamiko au adhabu zitakazotolewa na kamati ya ufundi na mashindano zita/yatasikilizwa na jopo la rufaa litakaloongozwa na;

a) Makamu Mwenyekiti
b) Mkurugenzi wa ufundi - Katibu
c) Mkurugenzi wa waamuzi kama mjumbe.
d) Wajumbe watatu (3) miongoni mwa wajumbe wa timu zinazoshiriki ligi wasiokuwa waalimu na wasiokuwa wa timu zinazo leteana mashitaka.
e) Mjumbe mmoja kutoka kamati ya maendeleo ya michezo ya mkoa husika.
f) Ikibidi mwakilishi wa TBF au TBF inaweza teua wajumbe wa kamati tofauti kukionekana kuna muingiliano wa maslahi wa aina yoyote.

23.2. Wajumbe wa jopo hili wanatakiwa wasiwe miongoni mwa walalimikaji / walalamikiwa, endapo itatokea hivyo italazimika wateuliwe wajumbe wengine kwa muda kusikiliza rufaa hiyo.
23.3. Timu/Klabu yoyote itatakiwa iwasilishe Rufaa yake si Zaidi ya siku tatu (3) baada ya maamuzi ya kamati ya ufundi kutolewa.
23.4. Kutakuwa na Ada ya Rufaa ambayo itapendekezwa na chama cha mkoa husika na Ada lazima Ziambatanishwe na barua ya rufaa.
23.5. Rufaa lazima iwe ya maandishi nakala tatu (3) zikiambatanishwa na vielelezo.
23.6. Hakuna fedha itakayo rudishwa hata timu/klabu itashinda rufaa.
23.7. Jopo la rufaa litasikiliza hoja na mawazo ya wawakilishi wa timu/Klabu kabla ya kutoa maamuzi ya rufaa hiyo.
23.8. Jopo la rufaa litatoa maamuzi baada ya kukaa na kuwasiliana na pande husika ndani ya siku tano baada ya rufaa kuwasilishwa katika chama cha mkoa husika.

23.9. Maamuzi ya ya jopo la rufaa ni ya mwisho. Pande husika zitajulishwa kwa maandishi maammuzi yaliyochukuliwa na jopo hilo.

23.10. Tukio lolote litakalothibitishwa na timu/Klabu kama ni sahihisho au kosa, bodi itarudisha kosa au sahihisho hilo kwa jopo la rufaa, ambalo litafanya uchunguzi na kutoa maamuzi ya tukio hilo.

## 24. UDHALILISHAJI WA NEMBO(BRAND), JINA LA CHAMA AU VYAMA VISHIRIKI NA MDHAMINI.

24.1. Kiongozi wa Klabu/Timu, Mchezaji, Mwalimu, Mwamuzi na mdau mwingine yeyote hatoruhusiwa kutukana na kuidhalilisha brand/nembo ya ligi ya mkoa, ligi ya taifa, mashindano ya kitaifa au wadhamini kwa kutoa takwimu za uongo kwenye mitandao ya kijamii kwa lengo la kupotosha na kuchochea chuki katika jamii ya wanakikapu.

24.2. Takwimu Sahihi itolewa na Viongozi wa Chama cha Mkoa husika, kama kuna walakini basi timu/Klabu, mwamuzi, mwalimu au mdau yeyote atapeleka kwa maandishi na viambatanisho kwa Mkurugenzi wa ufundi wa chama cha mkoa husika.

24.3. Ikibainika uchunguzi utafanyika na ushaidi kutolewa, faini ya kiwango husika kilichopangwa na chama husika kitatozwa kwa mhusika aliye fanya kitendo hicho.

24.4. Vyama vya mkoa, wanachama wake na wadau hawataruhusiwa kutumia nembo za TBF na wadau wake bila ya ruhusa ya kimaandishi kwa wakati wowote na shughuli yoyote.

## 25. USIMAMIZI/UTEKELEZAJI WA ADHABU

25.1. Usimamizi na utekelezaji wa adhabu utasimamiwa na Katibu au Mkurugenzi wa ufundi kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa. Waliopewa adhabu watapaswa kutumikia adhabu waliyopewa ndipo waruhusiwe kuendelea na michezo au kuanza msimu mwingine endapo msimu ulimalizika wakitumikia adhabu.

25.2. Hakutakuwa na haki ya kupinga dhidi ya tozo au adhabu zitakazo tolewa kwa timu/klabu, waalimu, wachezaji nk.

## 26. USIMAMIZI WA MCHEZO.

26.1. Viwanja vyote vitakavyotumika katika ligi na mashindano vitateuliwa na kamati ya ufundi baada ya kupendekezwa na Kurugenzi/kamisheni ya Ufundi na Mashindano na kuidhinishwa na bodi.

26.2. Michezo yote itachezwa kwa kufuata sheria za shirikisho la mpira kikapu ulimwenguni (FIBA) na kanuni za shindano zitawekwa na chama husika kwa kufuata Muongozo huu.

26.3. Chama na vilabu ambavyo viwanja vyake vitateuliwa na kupitishwa na bodi kutumika vinatakiwa kuwa na vifaa vyote vinavyotakiwa kutumika muda wa

mchezo. kama meza, viti vya kukalia wachezaji n.k. Kama uwanja huo utakua ni wa jumuiya basi viongozi usika watakao kuwepo wakisaidiana na Timu husika zitakua na jukumu la kuhakikisha eneo lina vifaa vya kutosha kukidhi mahitaji ya mchezo.

26.4. Baada ya mchezo kumalizika Kocha Mkuu/Msaidizi/Mtunza takwimu/Nahodha wa timu, kwa timu zilizocheza wanatakiwa kufika mezani kwa ajili ya kuchukuwa karatasi ya matokeo (score sheet). Meza haitahusika na uhifadhi wa karatasi ya matokeo ya timu.

26.5. Ni marufuku kwa mchezaji yeyote aliyesajiliwa na timu/klabu kusimamia au kuongoza benchi la timu/klabu nyingine inayoshiriki ligi ya Mkoa ya Wanawake au wanaume.

26.6. Mchezaji, kocha anaruhusiwa kusimamia au kuongoza bench la timu ambayo haishiriki ligi husika. Pia awe amesajiliwa kama kocha na akiwa na vyeti vinavyomruhusu kusimamia timu.

## 27. HUDUMA YA KWANZA NA AFYA

27.1. Chama cha mkoa husika kinawajibu wa kutoa huduma ya kwanza muda wote wa ligi. Lazima kuwe na daktari wa huduma ya kwanza kwenye kila mchezo nje ya daktari wa timu. Chama cha mkoa lazima kiwe na sanduku la huduma ya kwanza.

## 28. KUFUTA KANUNI NA MAMBO YASIYOKUWEPO KWENYE KANUNI

28.1. TBF ndiyo itakayohusika na ufutaji wa kanuni husika katika Ligi ya mkoa husika baada ya kupokea barua yenye maelezo kutoka kwa mkoa husika sababu nzito za kushindwa kuitumia kanuni au kipengele cha kanuni zilizo ainishwa na TBF.

28.2. Jambo/tukio lolote ambalo halikutajwa katika kanuni hizi, bodi ya ligi ikishirikiana na Kamisheni Husika ya TBF, itakuwa na maamuzi ya mwisho juu ya jambo/tukio hilo.

## 29. DOKEZO

TBF inaagiza kilabu, makocha, na waamuzi kuzisoma kwa makini kanuni hizi na kuhakikisha zinaeleweka na kufuatwa kwa faida ya mchezo wa mpira wa kikapu. TBF inapenda kuwakumbusha watu wote kuwa Basketball inalindwa na sheria pamoja na kanuni.

TBF inasisitiza Vilabu kuhakikisha kuwa kanuni hizi pia zinaeleweka vizuri kwa wachezaji na washabiki wake, kwani itasaidia kuwafanya wafahamu kanuni na taratibu za mpira wa kikapu vizuri na kwa kuzifahamu kanuni.

TBF siku zote itahakikisha mchezo wa mpira wa kikapu unakuwa na heshima kwa kusimamia kwa uadilifu kanuni na sheria za mchezo huu, kutoa adhabu inapobidi, kuelimisha na kuhakikisha siku zote mshindi anapatikana uwanjani kwa kufuata kanuni na taratibu za mchezo.

Mwongozo huu umetayarishwa na: -
**KAMISHENI YA UFUNDI NA MASHINDANO**